

Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili kwa Wageni

Sarah Vicent¹

Chuo Kikuu cha Dodoma

&

Arnold B. G. Msigwa²

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Ulimwengu wa utandawazi umesababisha kusambaa kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), hususani matumizi ya kompyuta na viambata vyake. Kwa hali hiyo, maendeleo yamesababisha kuenea kwa lugha zinazotumika katika teknolojia hiyo kama vile Kiingereza na lugha nyingine za Kimagharibi, na kwa kiasi kidogo, lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili. Hata hivyo, TEHAMA imekuwa ikitumiwa na walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia lugha za kigeni hasa Kiingereza kama inavyoelezwa na Lopez (2016), Bostina (2016), Bilyalova (2016). Aidha, zipo tafiti chache zilizozungumzia changamoto za kutumia Kiswahili katika TEHAMA, kwa ujumla, bila kuzungumzia namna Kiswahili kinavyoweza kutumika kiteknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji kwa wageni. Kwa hiyo, makala haya yamejadili suala hilo na yanajikita katika kufafanua umuhimu na changamoto za TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni. Aidha, makala haya yametoa mapendekezo ya nini cha kufanya ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji huo. Data zilizotumika katika makala haya zimepatikana kwa njia ya dodoso. Mkabala wa kitaamuli umetumika katika kuchambua data. Matokeo yamebaini kuwa kuna umuhimu wa kutumia TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwa wageni kwani inarahisisha ufundishaji kwa maana ya kutumia muda mfupi kufundisha mambo mengi. Pia, inamfanya mwanafunzi afurahie somo bila kuchoka na kupunguza gharama za ujifunzaji. Pamoja na umuhimu huo, zimebainika changamoto katika matumizi ya TEHAMA, yaani wakati mwingine wanafunzi wanapata shida kutumia matini zilizo mtandaoni kutokana na kukosa mwingiliano wa moja kwa moja na mwalimu, kukosekana kwa matini za kutosha na zilizoandikwa kwa usahihi mitandaoni, kukosekana kwa vifaa kama projekta na kompyuta na baadhi ya walimu na wanafunzi kutokuwa na maarifa ya kutosha ya matumizi ya vifaa hivyo. Kwa ujumla, makala yanahitimisha kwamba upo umuhimu wa kupendekeza mbinu zinazoweza kukabiliana na changamoto hizo kama vile kuwa na semina za mara kwa mara za kufundisha namna ya kutumia vifaa vinavyohusiana na TEHAMA, kuwa na vifaa vya kutosha na vinavyokidhi mahitaji ya

¹ Barua pepe: sarahvicent@yahoo.com

² Barua pepe: agawasike@gmail.com

ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni kwa kutumia TEHAMA kwenye taasisi za watu binafsi na taasisi za serikali.

1.0 Utangulizi

TEHAMA ni kifupi cha istilahi ‘Teknolojia ya Habari na Mawasiliano’. Maneno haya hili lina maana ya jumla inayorejelea mifumo yote ya kiteknolojia inayotumika kutengeneza, kuhifadhi, kuchakata na kutumia habari (Negoescu na Bastina-Bratu, 2016). Aidha, kwa upande mwingine, neno TEHAMA linarejelea mawasiliano ya kutumia simu, redio au televisheni ambayo husaidia katika upatikanaji wa matini, video na ishara za video na kuweza kusafirishwa mahali popote duniani ambapo ishara/taarifa za kidijiti huweza kupokelewa. Kwa ujumla, TEHAMA inajumuisha matumizi ya kidijiti ya vifaa na programu tumizi mbalimbali zenye uhusiano wa moja kwa moja na kompyuta katika matumizi yake. Vifaa na programu hizo ni kama vile projekta, mawasilisho yanayotumia programu ya *powerpoint*, matumizi ya programu za *skype* na *zoom* katika kufanya mikutano, matumizi ya blogu mbalimbali kama vile *www.edmondo.com*, *www.wordpress.com*, *www.wikispace.com*, kamusi za mitandaoni, vitabu vya mitandaoni, tovuti, programu zinazohusu michezo ya mitandaoni, *YouTube*, *WhatsApp*, *Instagram*, *Twitter*, matini za video na audio, baruapepe n.k. (Bate na Poole, 2003; Korlotyan, 2015; Bratu na Negoescu, 2016; Bilyalova, 2016; Lopez, 2016; Ahmadi, 2018 na Mofareh, 2019).

TEHAMA ni kiungo muhimu katika maendeleo ya watu duniani. Wanadamu wamekuwa wakitumia teknolojia hii katika kufanya mawasiliano muhimu katika nyuga mbalimbali kama vile siasa, biashara, uchumi, michezo, elimu, na kadhalika. Katika muktadha wa elimu, TEHAMA imekuwa ikitumika katika kufundishia na kujifunzia mambo mbalimbali yahusuyo jamii kama vile ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni. Hii ina maana kwamba walimu na wanafunzi wamekuwa wakijitahidi kuendana na mahitaji ya sasa ya jamii ambayo yamejikita zaidi katika matumizi ya sayansi na teknolojia na ambayo kwa namna moja au nyingine yamerahisisha ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na urahisi huo, walimu katika maeneo mengi ya dunia wamekuwa wakitumia teknolojia ya habari na mawasiliano wawapo darasani ili kufundisha kwa urahisi na ufasaha kwa lengo la kutimiza mahitaji ya wanafunzi (Bratu na Negoescu, 2016).

Ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA umekuwa ukifanyika kwenye masomo mbalimbali kama vile masomo ya sayansi na masomo ya sanaa. Ufundishaji huo umekuwa ukitoa matokeo chanya. Ahmadi (2018) anaeleza kwamba moja ya elementi muhimu katika ujifunzaji ni njia ambayo mwalimu anatomia darasani katika kuwezesha mchakato wa ujifunzaji lugha. Katika masomo ya sanaa, ujifunzaji wa lugha ya kigeni ni mojawapo ya masomo ambayo yamekuwa yakifundishwa na wajifunzaji wakijifunza kwa kutumia TEHAMA ambapo kompyuta imekuwa ikitumika kama kifaa muhimu cha kutolea maarifa hayo katika madarasa ya lugha. Tomlinson (2011) na Genelter (2015) wanaeleza kwamba kazi zinazohusisha matumizi ya kompyuta zinawapa wanafunzi matini

mbalimbali kwa haraka na kwa usahihi. Aidha, wanaendelea kueleza kwamba matini hizo zinamhamasisha mwanafunzi kujifunza zaidi.

Hata hivyo, tafiti mbalimbali kama vile za Maria (2012), Lopez (2016), Bilyalova (2016) na Osario (2017) zinaonesha kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa kutumia TEHAMA umefanyika zaidi kwa wajifunzaji wanaojifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya kigeni na lugha nyingine chache za Ulaya bila kuzungumzia lugha za Afrika. Pamoja na hayo, zipo baadhi ya tafiti ambazo zimezungumzia namna lugha ya Kiswahili ilivyoingizwa kwenye mfumo wa TEHAMA na changamoto zake bila kufafanua namna TEHAMA inavyosaidia katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni. Kwa hivyo, makala haya yameziba pengo hilo kwa kuchunguza namna TEHAMA inavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili hasa katika kubaini umuhimu na changamoto zake na kupendekeza mbinu za kukabiliana na changamoto katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni.

Data za makala haya zimepatikana kupitia utafiti mdogo uliofanyika katika maeneo ya Arusha na Zanzibar. Jumla ya watoataarifa sita (6) walishiriki katika utafiti huu katika mgawanyo ufuatao: kundi la kwanza limehusisha wanafunzi wawili (2) wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni na kundi la pili limehusisha walimu wanne (4) wanaofundisha Kiswahili kwa wageni kutoka kwenye vituo vifuatavyo: *Chuo cha MS Training Center for Development Cooperation* (MS-TCDC) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (CHUKITAZA). Katika mgawanyo huo wa watoataarifa, kila kituo kilihusisha walimu wawili na mwanafunzi mmoja. Idadi ya walimu imekuwa kubwa zaidi kwa sababu wana uzoefu wa kutosha katika suala la ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni kuliko wanafunzi. Aidha, data zimepatikana kwa kutumia mbinu ya dodoso na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli.

2.0 Nadharia ya Utafiti

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Mwingiliano wa Kijamii iliyoasisiwa na Vygotsky mwaka 1987. Wanamwingiliano wa Kijamii wanaamini kwamba ufanyaji kazi wa akili ya binadamu unafungamanishwa na maingiliano ya mfumo wa kiutamaduni uliopo katika jamii na taasisi za kijamii. Wanaona kuwa kujifunza lugha si mchakato wa mtu binafsi tu, bali hufungamana na mambo mengi ya kijamii na kiutamaduni. Hivyo, msingi wa kimazoea wa kiutamduni ndio unaozingatiwa katika makala haya. Nadharia hii iliibuka kutokana na udhaifu wa Nadharia ya Utabia na Nadharia ya Uhulka. Nadharia hizi zilikuwa zinaongoza ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni katika wakati huo. Nadharia hizo zilikuwa hazizungumzii namna ujifunzaji wa lugha ya kigeni unavyoweza kufanyika. Ilibainika kwamba tabia-mwigo peke yake na uwezo wa kuzaliwa wa kujifunza lugha haviwezi kutosheleza kumsaidia mjifunzaji kujifunza lugha na kumudu vizuri bali vihusishwe pia na mwingiliano baina ya wajifunzaji, walimu na wazungumzaji wazawa katika jamii husika. Long (1991) anashadidia mawazo ya Vygotsky kwa kueleza kwamba Nadharia ya Mwingiliano Jamii ni bora na ina nguvu kuliko nadharia nyingine kwa sababu imehusisha uwezo wa kuzaliwa wa

kujifunza lugha na mambo yanayohusiana na mazingira katika kuelezea suala la ujifunzaji wa lugha. Aidha, wanamwingiliano jamii wanaeleza kwamba maarifa ya ujifunzaji lugha yanapatikana kwanza kupitia mwingiliano wa watu katika jamii na baadaye kuingia katika mfumo wa akili wa mjifunzaji.

Katika kufafanua misingi ya nadharia hii, Vygotsky anaeleza kwamba wajifunzaji wana uwezo wa kujifunza lugha mpya kwa urahisi kupitia kuchangamana na jamii husika na kushiriki shughuli za kijamii. Hili linahusisha wajifunzaji, walimu na wazungumzaji wazawa wa lugha lengwa. Hii ina maana kwamba ni lazima ujifunzaji uhusishe tabia za kitamaduni za kijamii na uzoefu wa maisha ya mtu ya kila siku. Halikadhalika, nadharia hii inazingatia aina ya miingiliano inayofanyika baina ya wajifunzaji wa lugha ya kigeni. Kwa mfano, inasisitiza mwingiliano baina ya wazungumzaji wazawa na wasio wazawa (wajifunzaji) ambao unahusisha upatikanaji wa ingizo bora na la kutosha kwa wajifunzaji wa lugha.

Kwa hivyo, kutokana na ufafanuzi huo, nadharia hii imefaa kutumika katika kuongoza uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala haya kwa sababu katika maisha ya sasa ujifunzaji lugha umekuwa ukihusishwa kwa kiasi kikubwa na mwingiliano baina ya wajifunzaji na walimu na wazungumzaji wazawa kupitia TEHAMA. Mkabala wa kisasa wa ufundishaji lugha kimawasiliano unasisitiza ushirikishwaji wa mjifunzaji lugha katika matendo na shughuli mbalimbali za jamii lugha anayojifunza. Hii ina maana kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yamebadilisha kwa kiasi kikubwa mbinu ya ujifunzaji na ufundishaji lugha kutoka kwenye mwingiliano wa ana kwa ana (ambao unatumia mbinu za jadi) wa wajifunzaji katika jamii kwenda kwenye mwingiliano wa wanafunzi, walimu na jamii kupitia TEHAMA.

Aidha, kutokana na maendeleo hayo ni wazi kwamba tofauti na vitabu vilivyopo mtandaoni, matini nyingi zinazohusu ujifunzaji wa lugha zimekuwa zikirekodiwa na walimu na kuingizwa mtandaoni kupitia programu tumizi mbalimbali kama vile kupitia mtandao wa *Youtube*, kupitia majukwaa na blogu mbalimbali. Matini hizo zimekuwa zikiwasaidia wanafunzi kujifunza lugha ya kigeni kwa urahisi zaidi bila kumtegemea mwalimu. Hii inadhihirisha kwamba katika zama hizi za sayansi na teknolojia ujifunzaji wa lugha ya kigeni unahusisha pia mwingiliano wa moja kwa moja baina ya mwanafunzi na TEHAMA. Pamoja na mwingiliano wa wanafunzi na TEHAMA katika kujifunza mwalimu pia anaweza kutumia vifaa vinavyohusiana na TEHAMA darasani akiwa na wanafunzi na kusaidia ujifunzaji kuwa wa haraka na rahisi.

3.0 Matumizi ya TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Lugha ya Kigeni Kwa Ujumla

Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni yameleta mapinduzi makubwa kwa kuwezesha upatikanaji rahisi wa maarifa kwa wanafunzi wanaoishi mijini na vijijini. Ama kwa upande mwingine, mabadiliko hayo yamewasaidia wanafunzi waweze kujifunza kwa kujitegemea (Mexhuani,

2014). Tafiti nyingine zimeonesha kuwa matumizi ya TEHAMA katika kuwezesha suala la elimu hasa kupitia mtandao wa intaneti, yamechangia kwa haraka katika kukuza na kuendeleza mchakato wa uamiliaji na ujifunzaji wa lugha ya kigeni. Aidha, matumizi hayo ya TEHAMA yamewezesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kupitia utumiaji wa daimensheni mpya ya vifaa inayohusisha mfumo wa intaneti kama vile kompyuta, *tabulate*, n.k. (Erben, Ban na Castaneda, 2009).

Kwa mujibu wa Paulsen (2001) matumizi mazuri ya matini za mtandaoni yanaweza kutoa matokeo chanya kwa wajifunzaji kwa namna sawa na jinsi ambavyo mjifunzaji huyo angejifunza katika mazingira halisi ya lugha hiyo na utamaduni wake nje ya nchi yake. Hii inamaanisha kwamba kujifunza lugha kwa kutumia matini zinazofungamanishwa na TEHAMA hakuna tofauti na kujifunza lugha husika katika mazingira halisi. Paulsen (*keshatajwa*) anaendelea kueleza kwamba sababu kubwa ya kutoa matokeo chanya ni uhalisia wa matini zenyewe na motisha ya kutumia matini hizo kutokana na uhalisia huo. Hata hivyo, pamoja na maoni ya Paulsen (*khj*) ni wazi kwamba kujifunza lugha katika mazingira halisi ni tofauti na kujifunza lugha kupitia TEHAMA kwa sababu kwa kutumia TEHAMA hata kama matini zina uhalisia wakati mwingine mwanafunzi anaweza kuwa anahitaji kuuliza swali au kupata ufafanuzi wa jambo fulani akashindwa lakini akiwa kwenye mazingira halisi anaweza kuuliza na kupata majibu wakati huohuo.

Kwa upande mwingine, Thorne (2010) anaeleza kwamba ingawa teknolojia inayohusiana na mtandao wa intaneti ina mfumo kazi unaofanana katika nchi nyingi, utofauti upo katika utamaduni wa matumizi ya mfumo huo. Hii inatokana na namna teknolojia inavyochukuliwa katika miktadha tofauti ya kijamii. Katika muktadha wa ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya kigeni kimataifa, imebainika kwamba kuna matumizi makubwa na ya aina tofautitofauti ya mawasiliano ya kielektroniki na ambayo wakati mwingine yanasababisha ugumu kwa watumiaji ambao hawana utamaduni wa kutosha wa kutumia mifumo hiyo. Hii inadhihirisha kwamba ipo changamoto katika matumizi ya TEHAMA kwa wafundishaji na wajifunzaji wa lugha ya kigeni kwani wakati mwingine mwanafunzi anakuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kutumia teknolojia kuliko mwalimu, jambo ambalo linaweza kuzuia mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji kufanyika kwa ukamilifu. Hali ya wanafunzi kuwa na ufahamu zaidi katika matumizi ya teknolojia imeelezwa pia na Prensky (2001) kwamba wanafunzi wa zama hizi wamebadilika sana katika matumizi ya mbinu tofauti tofauti za ujifunzaji kwani inaonekana kwamba wanafunzi hao wapo tofauti na mfumo wa elimu ambao uliandaliwa kwa ajili yao. Hii ina maana kwamba walimu wanapaswa kubadili mbinu wanazotumia kufundishia ama kuchanganya mbinu walizokuwa wakizitumia zamani na mbinu za sasa ili ujifunzaji na ufundishaji ufanyike kwa ubora zaidi.

4.0 Umuhimu na Changamoto za TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kwa Wageni

Lengo kuu la utafiti uliozaa makala haya ni kubainisha umuhimu wa kutumia TEHAMA kwenye ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Aidha, malengo mengine mahususi yalikuwa ni kufafanua changamoto za utumiaji

wa TEHAMA katika kufundishia Kiswahili na mapendekezo ya mbinu za kukabiliana na changamoto hizo. Imebainika kwamba ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutumia TEHAMA una umuhimu, lakini pia una changamoto ambazo zimefafanuliwa katika kipengele namba 4.1 na 4.2, mtawalia. Kadhalika, mapendekezo ya mbinu za kukabiliana na changamoto hizo yamefafanuliwa katika kipengele namba 5.0.

4.1 Umuhimu wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni

Utafiti uliozalisha makala haya umebaini kwamba upo umuhimu wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni kama ulivyobainishwa hapa chini: katika jedwali Na 1.1 hapa chini na kutolewa ufafanuzi katika sehemu inayofuata.

Mosi, TEHAMA hurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Katika hoja hii imeelezwa kwamba, matumizi ya TEHAMA yanarahisisha ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa namna tofautitofauti. Kwanza ni kupitia matumizi ya *powerpoint*/projekta. Matumizi ya projekta yanahusisha uandaaji wa nukuu za somo katika mfumo wa maunzi laini katika kompyuta na kuziweka katika mtindo wa dondoo ili kuziwasilisha kwa wanafunzi kwa urahisi. Walimu ambao wamekuwa wakitumia vifaa hivyo wameeleza kwamba mtindo wa dondoo umewasaidia kufundisha mambo mengi kwa haraka na kwa muda mfupi. Hii inamwezesha mwalimu kukamilisha mada alizopaswa kufundisha ndani ya muda aliopangiwa mwanafunzi wake. Ama kwa upande mwingine watoatarifa wameeleza kuwa TEHAMA imekuwa ikiwasaidia walimu kumaliza kufundisha kabla ya muda wa mwanafunzi kuisha. Jambo hili linampa mwalimu nafasi ya kutosha ya kufanya marudio kwa wanafunzi wake kwa kuwapa mazoezi ya kutosha na kuufanya ufundishaji kuwa wa manufaa zaidi kwa wanafunzi.

Pia, matumizi ya TEHAMA hurahisisha ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa sababu mwalimu anaweza kuwafundisha wanafunzi wake hata wakiwa nje ya nchi au mahala popote ambapo hawawezi kuonana ana kwa ana. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwa na darasa la wanafunzi kutoka Marekani na akawa anafundisha bila kukutana nao ana kwa ana. Hii ina maana kwamba mwalimu anaweza kuwasiliana na wanafunzi hao kupitia mitandao ya kijamii kama vile; *WhatsApp*, *Youtube*, *Instagram* n.k. Katika mawasiliano hayo, mwalimu anaweza kuwafundisha wanafunzi wake bila kikwazo kwani anaweza kuunda kundi linalomjumuisha yeye na wanafunzi wake, kisha wakawa wanajadili mada mbalimbali zinazohusiana na lugha ya Kiswahili. Yaani, mwalimu anaweza kuandaa somo na kulifundisha kupitia kundi la *whatsapp* au anaweza kuandaa somo kwa kujirekodi na kuliweka kwenye mtandao wa *Youtube* na kuwataka wanafunzi wasome kupitia mtandao huo.

Vilevile, ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni kwa kutumia TEHAMA umerahisishwa kupitia programu za *skype* na *zoom* ambapo mwalimu na

wanafunzi wanaonana na kuzungumza mtandaoni. Programu tumizi hizi humwezesha mwalimu kufundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja hata kama wapo kwenye nchi tofauti. Kwa hivyo, ili kumfundisha mwanafunzi wa kigeni lugha ya Kiswahili si lazima mwanafunzi huyo aje nchini Tanzania au mwalimu aende kumfundisha nchini mwake. Aidha, katika kusisitiza hilo, walimu kutoka MS-TCDC walionesha kufurahia kuendelea kwa madarasa yao kupitia programu hizi tumizi wakati wa mlipuko wa UVIKO-19. Ama kwa upande mwingine tunaweza kusema kwamba hoja hii inaenda sambamba na hoja ya kurahisisha mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi kwa maana kwamba muda wowote mwalimu anaweza kuwasiliana na mwanafunzi jambo ambalo linafanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa rahisi.

Pili, TEHAMA humsaidia mwanafunzi kuelewa dhana iliyokusudiwa na mwalimu. Hoja hii imefafanuliwa kwamba, wakati mwingine mwalimu anaweza kuwa anafundisha mada fulani lakini ikaonekana kutokueleweka kwa urahisi kwa wanafunzi hasa dhana zihusuzo masuala ya kiutamaduni ikiwa hakutumia njia shirikishi za kisasa. Kwa mfano, ikiwa mwalimu anafundisha mada za kitamaduni kama vile jando na unyago, kwa mwanafunzi ambaye hana ufahamu juu ya mambo hayo anaweza kupata shida kuzielewa mada hizo. Kwa hivyo, ili mwanafunzi aweze kuzielewa mada hizo mwalimu anaenda kwenye sherehe za jando na unyago na kurekodi matukio muhimu yanayofanyika kwa kutumia *Digital Video Disc* (DVD). Baada ya kurekodi mwalimu anawapa wanafunzi ili waweze kuangalia matukio hayo ambayo yamefanyika katika mazingira halisi. Wanafunzi wakishaangalia matukio hayo na simulizi zinazoambatana na hayo matukio katika DVD, huwasaidia kuelewa mada ambazo mwalimu anazifafanua. Hii inathibitisha kwamba ufundishaji huu umekuwa ukimsaidia mwanafunzi kuelewa dhana hizo kwa mapana zaidi. Hoja hii imezungumzwa pia na Bilyalova (2017) anapoeleza kwamba matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa ujifunzaji yanaelekezwa kumzamisha mwanafunzi kwenye mazingira ya lugha ambayo yanachangia katika kukuza umilisi wake wa uzungumzaji hasa katika kipengele cha utamaduni.

Tatu, TEHAMA humsaidia mwalimu kwenda na wakati kwa kujifunza zana mbalimbali za kisasa zinazotumika kufundishia. Izingatiwe kwamba TEHAMA inahusisha matumizi ya mbinu tofauti na zile zilizokuwa zikitumika awali. Kabla ya maendeleo ya TEHAMA walimu wa lugha ya kigeni walikuwa wakitumia mbinu za asili za kufundishia kama vile ufundishaji wa ana kwa ana wa mwalimu kwa wanafunzi, matumizi ya vitabu na notisi zilizokuwa katika mfumo wa maunzi ngumu, vikundi vya majadiliano ndani ya darasa, kutafsiri msamiati n.k. Matumizi ya TEHAMA yamekuwa yakihusisha vifaa na mbinu za kisasa katika kufundishia na kujifunzia lugha ya kigeni kama vile: intaneti, *zoom*, *skype* na michezo ya lugha. Kwa hivyo, teknolojia hiyo imesababisha mwalimu wa lugha ya kigeni kujifunza mbinu anuwai za kufundishia kama vile kufundisha kwa kutumia programu ya *powerpoint* ambayo inahusisha vifaa kama vile kompyuta na projekta. Kadhalika, TEHAMA imesaidia mwalimu kujifunza ufundishaji kwa kutumia programu za *skype* na *zoom* namna ya kutumia aipadi (*Ipod*) kama kifaa cha kufundishia, namna ya kuandaa programu zinazohusisha michezo mbalimbali

ya kujifunzia. Pia, TEHAMA imemsaidia mwalimu kuwa kwenye mazingira ya kujua namna ya kuwafundisha wanafunzi wake kupitia mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp*, *Facebook*, *Instagram* na *Twitter* na namna ya kuzifungua akaunti hizo. Kwa hivyo, matumizi ya TEHAMA yamemsaidia mwalimu kwenda na wakati na kuwa mtu wa kujifunza zaidi ili aweze kuwasiliana na wanafunzi wake kupitia mifumo ya KiTEHAMA kama ilivyofafanuliwa katika hoja hii.

Nne, TEHAMA huongeza hamasa ya usomaji kwa mwanafunzi. TEHAMA humfanya mwanafunzi kuwa na hamasa ya usomaji darasani. Kwa kuzingatia hoja ya hamasa, uzoefu wa walimu katika madarasa yao ya lugha umeonesha kwamba mwanafunzi anajifunza kwa kuhamasika zaidi mwalimu anapotumia picha, video na matini za kusikiliza (*audio*) ambazo hazihusishi sauti ya mwalimu. Hii inamfanya mwanafunzi ajifunze katika hali ya uhai zaidi bila kuchoka. Kwa mfano, Msigwa (2019) anaeleza kwamba video nzuri na zenye ucheshi huwasukuma wajifunzaji lugha ya Kiswahili kupenda kujifunza lugha hiyo tofauti na ujifunzaji pasipo kutumia media za video. Kwa muktadha huo, wanafunzi huwa makini kufuatilia kile wanachojifunza kutokana na kuvutiwa na picha, video pamoja na sauti zinazoambatana na picha hizo. Kadhalika, TEHAMA humfanya mjifunzaji ajifunze kwa kutenda na hivyo kumwondolea uchovu; yaani “ujifunzaji kwa kutenda”. Njia hii humfanya mwanafunzi kuhusisha zaidi matumizi ya viungo vya mwili na akili katika kutafuta matini za kujifunzia. Katika hoja hii TEHAMA inamtaka mwanafunzi kutumia muda mwingi kwenye kompyuta. Kwa hiyo, inamlazimu mwanafunzi kutumia akili na umakini katika kupakua matini mbalimbali zinazohusiana na lugha anayojifunza. Aidha, wakati mwingine mwanafunzi aliye mbali na mwalimu wake anahitajika kufanya mawasiliano naye kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii kama *WhatsApp*, *Facebook* au *Instagram* jambo ambalo linamtaka mwanafunzi kuwa hai ili aweze kuelewa kile anachofundishwa na mwalimu kwa wakati huo na kuweza kufanya mazoezi atakayopewa baada ya kipindi. Mtindo huu wa ufundishaji unamtaka mwanafunzi awe na hamasa ya usomaji na utulivu katika kutumia muda vizuri kwani baada ya kipindi anaweza kushindwa kumpata mwalimu mtandaoni.

Aidha, wakati mwingine mwalimu anaweza akaandaa michezo mbalimbali inayohusiana na ujifunzaji wa lugha kwa kutumia programu maalumu katika kompyuta. Michezo hiyo inamtaka mwanafunzi awe na hamasa ya usomaji kwani inahusisha maswali ya kuchagua jibu sahihi na kumtaka mwanafunzi kujibu ndani ya muda mfupi. Kwa hivyo, ujifunzaji huo ambao unamhusisha mwanafunzi moja kwa moja haumpi nafasi ya kuchoka bali kuwa mchangamfu/hai na kuendelea kujifunza kwa ajili ya kutimiza malengo yake.

Tano, TEHAMA hupunguza utegemezi wa ujifunzaji. Kwa kuzingatia hoja hii TEHAMA humjengea mwanafunzi uwezo wa kujitegemea (kujifunza peke yake). Hili limeelezwa na watoataarifa kutoka katika vituo vyote viwili, yaani CHUKITAZA na MS-TCDC kwamba TEHAMA huwajengea wanafunzi uwezo wa kujitegemea. Matumizi ya mtandao wa intaneti kwa kiasi kikubwa hufanywa na

wanafunzi. Hii ina maana kuwa muda mwingi mwanafunzi anakuwa peke yake na kompyuta yake akitafuta matini mbalimbali kwa ajili ya kujifunzia kupitia mtambo tafutizi wa *google*. Mtambo humsaidia mwanafunzi kuzifikia linki nyingine kama vile *Youtube*, blogu mbalimbali na tovuti zinazotoa mafunzo ya lugha na hivyo kupata uelewa mkubwa wa yale anayojifunza. Kama ilivyoelezwa mahala pengine katika makala haya, mwalimu anaweza akawa anaishi Tanzania na mwanafunzi Marekani. Katika masafa hayo, kazi ya mwalimu ni kutoa mafunzo kwa kiasi kidogo na kumpatia mwanafunzi kazi za kutosha ambazo zitamshughulisha mtandaoni ili aweze kujibu kwa ufasaha. Kwa hivyo, hii inathibitisha kwamba kupitia ujifunzaji wa kutumia TEHAMA mwanafunzi anajengewa uwezo na utamaduni wa kujifunza peke yake kwa kiasi kikubwa bila kumtegemea mwalimu au mwanafunzi mwenzake. Matokeo ya jambo hili ni kuzalisha wanafunzi wenye ufahamu huru.

Sita, TEHAMA huhamasisha ushirikiano katika ujifunzaji. Watoataarifa wote sita walioshiriki katika utafiti huu walibainisha kuwa TEHAMA hukuza ushirikiano katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha ya kigeni. TEHAMA kama ilivyofafanuliwa awali, imehamasisha ushirikiano baina ya mjifunzaji na mjifunzaji, baina ya mjifunzaji na mwalimu na pia baina ya mjifunzaji na wazungumzaji wazawa wa lugha anayojifunza. Ushirikiano baina ya mjifunzaji na mjifunzaji unajitokeza kutokana na asili ya ujifunzaji wenyewe. Hii ina maana kwamba kwa kuwa ujifunzaji lugha kwa njia ya TEHAMA unahusisha mwingiliano baina ya mwanafunzi na teknolojia, inamlazimu mwanafunzi anayejifunza kwa kutumia TEHAMA katika nchi fulani (mfano China) awe na ushirikiano na mwanafunzi anayesoma kwa njia ya mtandao nchi nyingine (mfano Uholanzi, Tanzania n.k.) Utaratibu huu umebainika kuwasaidia wanafunzi hao kupeana baadhi ya matini ambazo kila mmoja anakuwa amezipata katika utafutaji wake. Pia, huelekezana kimtandao (kwa maana ya kutumia *WhatsApp*, *baruapepe*, *Instagram* n.k.) baadhi ya mambo ambayo yanaonekana kuwa magumu kuyaelewa. Pia, mtoataarifa kutoka MC-TCDC alieleza kuwa ushirikiano huu umebainika kupitia michezo mbalimbali inayohusu ujifunzaji wa lugha ambayo inaingizwa kwenye programu maalumu kama vile programu ya “*kahoot*”. Kwa mfano, mwalimu anaweza akaandaa mchezo wa maswali unaohusisha aina za salamu kama vile salamu za watoto, salamu za vijana na salamu za watu wazima na kuwataka wanafunzi hao waoneshe tofauti za salamu hizo kwa kujibu maswali yaliyo katika mfumo wa kuchagua jibu sahihi. Katika kuonesha ushirikiano huo, kazi ya mwalimu ni kuachilia swali kwenye projekta na wanafunzi kujibu ndani ya sekunde chache na kutoa matokeo kwa wakati huohuo. Hivyo, kwa hoja hii TEHAMA inamfanya mwanafunzi awe huru na karibu na mwalimu wake jambo ambalo linamsaidia kuelewa kwa urahisi kile anachojifunza.

Halikadhalika, matumizi ya TEHAMA yamehamasisha ushirikiano baina ya mwanafunzi na mzawa wa lugha anayojifunza mwanafunzi kwa kiasi fulani. Hii ni kutokana na kuwa wakati mwingine mwanafunzi analazimika kufanya mawasiliano na wazungumzaji wazawa ili kuweza kupata taarifa mbalimbali zinazohusika na masuala ya kitamaduni. Kipengele cha utamaduni katika ujifunzaji

wa lugha ya kigeni ni kigumu kueleweka ikilinganishwa na vipengele vingine. Hivyo, mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kigeni hulazimika kupata taarifa nyingine za ufafanuzi kutoka kwa wazawa wa lugha ya Kiswahili. Hali hii inatokana na ukweli kwamba kwa mwanafunzi anayejifunza mtandaoni ni vigumu kuelewa baadhi ya istilahi za kitamaduni zinazotumika katika mfumo huo wa intaneti. Kwa hivyo, mwanafunzi analazimika kutafuta linki itakayomkutanisha na wazungumzaji wazawa ili aweze kukabili tatizo hilo. Jambo hili linazungumziwa pia na Dedja (2015) pale anapoeleza kwamba mwanafunzi anaweza kutembelea linki muhimu zinazohusu masuala ya kitamaduni au kuwasiliana na mzungumzaji mzawa kupitia chati, jukwaa, baruapepe, *skype* n.k., ili kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na utamaduni bila kukutana na mzungumzaji mzawa ana kwa ana. Taarifa hizi humsaidia pia kupata ujuzi wa kusoma na kuandika bila vikwazo.

4.2 Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kwa Kutumia TEHAMA

Miongoni mwa lengo mojawapo la utafiti uliozaa makala haya lilikuwa ni kufafanua changamoto zinazoambatana na matumizi ya TEHAMA katika kufundishia Kiswahili kwa wageni. Sampuli ya walimu na wanafunzi kutoka maeneo yaliyoteuliwa ilishiriki katika kutoa matokeo ya lengo hili. Data zinaonesha kwamba zipo changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili walimu na wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA kama zinavyobainishwa hapa chini:

Mosi, uhaba wa vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia TEHAMA ni kama vile kompyuta, projekta, simu maizi, *Ipod* na *tabulate*. Vifaa hivi ni muhimu na pengine vya lazima katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa kutumia TEHAMA. Hii ni kwa sababu, licha ya kwamba ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA unamhusisha mwanafunzi na TEHAMA, ufundishaji kwa kutumia TEHAMA unamhusisha mwalimu, mwanafunzi na vifaa vya kujifunzia vinavyohusika na TEHAMA. Ufundishaji huu unaweza kufanyika darasani au nje ya darasa kimtandao ambao pia unamtaka mwalimu na mwanafunzi kuwa na vifaa hivyo vya kufundishia na kujifunzia. Katika utafiti huu, walimu wote wanne kutoka vituo vyote vilivyoshiriki katika utafiti huu, wamebainisha changamoto ya uhaba wa vifaa. Hoja hii imefafanuliwa kwamba wakati mwingine ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA unakuwa mgumu kwa sababu ya kukosekana kwa vifaa. Katika CHUKITAZA, kwa mfano, walimu walibainisha kwamba hakuna uwiano baina ya idadi ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili chuoni kwao na idadi ya vifaa vya TEHAMA vya kujifunzia kama vile: kompyuta, *Ipod* na *tabulate*. Hii ina maana kwamba mwalimu anaweza akawa na darasa lenye wanafunzi wengi kuliko vifaa vilivyopo. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwa na darasa lenye wanafunzi 15 na wakati huohuo ana kompyuta 2 au 3 za kufundishia. Ufundishaji wa darasa hili unakuwa mgumu kwa sababu uwiano wa kompyuta 3 na wanafunzi 15 ni mdogo sana kwani hata kwa kushirikiana inakuwa ngumu.

Aidha, ni muhimu kuwa na kompyuta za kutosha katika darasa la lugha kwani hiki ni kifaa msingi ambacho kinamwezesha mwanafunzi kutumia mtandao wa intaneti kwa ajili ya kutafuta matini mbalimbali za kujifunzia. Hata hivyo, watoataarifa kutoka CHUKITAZA walieleza kwamba pengine, darasa la BETRASI (darasa maalumu linalojengwa kwa kuzingatia mifumo yote ya kiTEHAMA kwa ajili ya kufundishia wanafunzi wageni) likikamilika litasaidia kwa kiasi kupunguza changamoto hiyo.

Pia, ni muhimu kwa mwalimu kuwa na kompyuta kwani itamsaidia kupata matini za kutosha kwa ajili ya kufundishia na kuingiza programu zinazohusisha michezo mbalimbali ya lugha ambayo inamsaidia mwanafunzi kufahamu dhana mahususi katika mada fulani. Kadhalika, kukosekana kwa vifaa vingine kama projekta, *Ipod*, *tabulate* na simu maizi vinasababisha ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA kuwa mgumu. Kwa mfano, simu maizi zina uwezo wa kuunganishwa na mtandao wa intaneti na kumwezesha mwanafunzi na mwalimu kupakua matini mbalimbali za kujifunzia na kufundishia kadiri wanavyoweza na kukubaliana juu ya nini cha kufanya katika matini hizo. Kukosekana kwa kifaa hiki kwa mwalimu au mwanafunzi kumesababisha ufundishaji na ujifunzaji kuwa mgumu kwa kukosa mawasiliano na wanafunzi waliopo nje ya nchi au ndani ya nchi husika.

Pamoja na hayo, watoataarifa hao walifafanua zaidi kwamba mwalimu anaweza kuwa na baadhi ya vifaa na wanafunzi wake wakawa hawana. Pia, mwalimu anaweza kukosa baadhi ya vifaa na wanafunzi wakawa wanavyo jambo ambalo pia linaleta ugumu katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA. Ama kwa upande mwingine gharama za kununulia vifaa hivyo ni changamoto ambayo inasababisha kuwa na vifaa visivyotosheleza kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Halikadhalika, baadhi ya ‘aplikesheni’ ambazo zinaweza kutumika mtandaoni kwa ajili ya kujifunzia lugha ni gharama kubwa kiasi cha kushindwa kununuliwa kutokana na uchumi wa nchi, taasisi au wa mtu binafsi kuwa kwenye kiwango cha chini. Vilevile, watoataarifa kutoka MS-TCDC walieleza pia changamoto hizo za kukosekana kwa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia jambo ambalo limesababisha programu ya ufundishaji na ujifunzaji Kiswahili kwa wageni kwa kutumia TEHAMA kushindwa kufanyika kwa kiwango kinachotakiwa.

Pili, kukosekana kwa miundombinu thabiti kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Hoja hii imeelezwa kwamba ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA unahitaji miundombinu kama vile umeme na mtandao wa intaneti. Miundombinu hii inapaswa kuwa thabiti na ya uhakika ili mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji usikwame. Katika nchi maskini au nchi zinazoendelea, miundombinu kama nishati ya umeme si ya uhakika sana kutokana na uzalishaji wake kuwa mdogo. Uzalishaji huo unatokana na uwezo mdogo wa kuzalisha umeme wa kutosha, jambo ambalo linasababisha mgawo wa umeme huo maeneo mbalimbali. Mgawanyo huo unasababisha kupatikana na kukosekana kwa umeme kwa baadhi ya maeneo na kwa nyakati tofautitofauti. Kutokana na mgawo huo, nishati ya umeme inakuwa si thabiti na kusababisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA

kushindwa kuendelea kwani matumizi ya kompyuta, *Ipod*, *tabulate* na simu maizi yanategemea zaidi nishati hiyo.

Ama kwa upande mwingine, mtandao wa intaneti nao umekuwa ni changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA. Mtandao wa intaneti ndio unaomwezesha mwalimu na wanafunzi kupakua matini mbalimbali za kufundishia na kujifunzia kwa kutumia kompyuta au pia kuwasiliana kupitia mitandao mingine kama *WhatsApp*, *Facebook*, *Youtube*, baruapepe n.k. Wakati mwingine mtandao huo hukatika na kumfanya mwalimu na mwanafunzi washindwe kuendelea na somo, na pia wakati mwingine mtandao huo unakuwa chini sana kiasi ambacho unasababisha mwalimu akose uhuru wa kufanya kazi yake ya ufundishaji kwa urahisi. Hali hii inamlazimisha mwalimu kuusubiri mtandao kwa muda mrefu, jambo ambalo linampotezea muda na kumfanya ashindwe kutimiza malengo ya somo kwa siku hiyo. Pia, baadhi ya watoaarifa walieleza kwamba kukosekana kwa fedha za kununua vifurushi kwa ajili ya kuunganisha mtandao wa intaneti kwa baadhi ya walimu na wanafunzi ni changamoto katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia TEHAMA. Kutokana na hali duni kiuchumi kwa baadhi ya walimu hasa kwenye nchi zinazoendelea, hawana fedha kwa ajili ya kununua vifurushi hivyo. Suala hilo husababisha ujifunzaji na ufundishaji kuwa mgumu. Kevogo (2017) katika utafiti wake anadokeza kuhusiana na hoja hii kwa kueleza kwamba watu wengi barani Afrika hawawezi kumudu gharama ya huduma ya intaneti pale inapohitajika na pia ukosefu wa nishati ya umeme ni wa kiwango kikubwa hali inayokwamisha matumizi ya kompyuta.

Tatu, walimu kutokuwa na ujuzi wa kutumia TEHAMA. Kama ilivyofafanuliwa awali, TEHAMA ni teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo inahusisha matumizi ya kompyuta kwa kiasi kikubwa na vifaa vingine kama simu maizi, *tablate*, na aipadi yanayohusisha mtandao wa intaneti. Katika vifaa hivyo, hasa kompyuta mwalimu anapaswa kuzifahamu programu mbalimbali ambazo zitawezesha ufundishaji wake wa kutumia TEHAMA. Programu hizo ni kama vile za *Microsoft Word*, *Microsoft Exel*, *Microsoft Powerpoint* ambazo zinaenda sambamba na matumizi ya projekta, programu ya *skype*, programu ya *zoom* na namna ya kuutumia mtandao wa intaneti katika vifaa hivyo. Pamoja na kuwa imeelezwa katika kipengele cha umuhimu kuwa TEHAMA inampa mwalimu hamasa ya kujifunza mifumo mbalimbali ya kiteknolojia ili kwenda na wakati, utafiti umebainisha pia kwamba upataji huo wa maarifa ya TEHAMA ni wa polepole sana kiasi ambacho bado unaacha mwanya katika ufahamu wa matumizi vifaa vinavyohusiana na TEHAMA. Hii ina maana kwamba baadhi ya walimu wanakosa maarifa kamili ya kutumia vifaa na programu mbalimbali zinazohusiana na TEHAMA, jambo ambalo linasababisha ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia TEHAMA kuwa mgumu. Kwa mfano, wakati mwingine mwalimu anashindwa kutumia ‘aplikesheni’ mbalimbali za simu maizi kama vile *WhatsApp*, *Instagram*, *Facebook* na *Youtube* kutokana na ufahamu mdogo wa ‘aplikesheni’ hizo.

Halikadhalika, kutokana na ujifunzaji wa polepole wa mifumo ya kiteknolojia kwa walimu, imebainika kwamba baadhi yao hasa wanaofundisha Kiswahili kwa wageni wanashindwa kutumia mifumo hiyo katika ufundishaji, jambo ambalo linasababisha ufundishaji kwa kutumia TEHAMA kuwa mgumu. Kwa mfano, walimu hao hawapendi na hawajui kutengeneza *slides* za *power point* na pia kutumia projekta kufundishia. Hii ni kutokana na ufahamu mdogo wa kutumia kifaa hicho; wakati mwingine inapowalazimu kukitumia inawachukua muda mrefu kuunganisha kifaa hicho na kompyuta, jambo ambalo linachukua muda mrefu na kumsababishia mwalimu kushindwa kufikia malengo yake ya ufundishaji kwa siku hiyo. Pia, imebainika kwamba baadhi ya walimu hawana ufahamu wa kutosha kwenye matumizi ya ‘aplikesheni’ mbalimbali zinazotumika katika simu maizi ambazo ni muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha. Kwa mfano, kumekuwa na changamoto zinazowakumba walimu katika namna ya kuunda makundi ya *WhatsApp* kwa ajili ya kuwasiliana kimasomo na wanafunzi wao, namna ya kuwasiliana na mwanafunzi kupitia ukurasa wake wa *Instagram*, *Facebook*, namna ya kuingiza matini za kujifunzia kwenye aplikesheni ya *Youtube* n.k. Pia, imebainika kwamba ufahamu wa walimu katika matumizi ya programu za *skype* na *zoom* ambazo zinahusisha muonano wa macho kwa macho wa kielektoniki kati ya mwalimu na mwanafunzi ni mdogo zaidi jambo ambalo linaendelea kuthibitisha uwepo wa changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa kutumia TEHAMA.

Nne, matumizi ya vifaa visivyokidhi mahitaji ya kiTEHAMA. Imeelezwa kwamba kompyuta ni kifaa muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia TEHAMA. Katika mchakato huo mwalimu na wanafunzi wanapaswa kuwa na kompyuta zinazoendana na wakati uliopo na zinazoweza kukamilisha zoezi la ufundishaji na ujifunzaji kwa ufasaha. Ikiwa kompyuta zao zinatofautiana kimatoleo, zitakwamisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji lugha. Utafiti uliozaa makala haya umebaini kwamba wakati mwingine walimu wanakuwa na kompyuta ambazo ni za toleo la zamani sana na wanafunzi wanakuwa na kompyuta za kisasa. Kutokana na vipindi tofauti ambavyo kompyuta hizo zilizalishwa ni dhahiri kwamba zitakuwa na programu tofauti na hivyo kutokukubaliana kimatumizi jambo ambalo linakwamisha ujifunzaji na ufundishaji wa lugha.

Aidha, matumizi ya simu maizi nayo yameonekana kuwa ni muhimu katika kufanikisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Simu hizi zinapaswa kuwa na uwezo mkubwa kwa ajili ya kuingiza programu/aplikesheni mbalimbali ambazo zinaweza kufaa katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Aplikesheni hizo ni kama vile *WhatsApp*, *Facebook*, *Youtube*, *baruapepe*, *Instagram* n.k. Makala haya yamebaini kwamba baadhi ya simu zinazotumiwa na walimu na wanafunzi zina uwezo tofauti wa kupakua aplikesheni hizo ambapo nyingine zinakuwa na uwezo wa kupakua aplikesheni nyingi na nyingine zinakuwa na uwezo mdogo. Hali hii inasababisha walimu na wanafunzi kuwa na simu ambazo hazikidhi matumizi kamili ya TEHAMA na hivyo kusababisha zoezi la ufundishaji na ujifunzaji kupwaya. Kwa mfano, ujifunzaji na ufundishaji kupitia *WhatsApp*,

baruapepe na *Youtube* unafanyika kwa kiwango kikubwa, kwa hivyo, ikiwa simu mojawapo kati ya simu ya mwalimu au ya mwanafunzi inakosa aplikesheni hizo mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia TEHAMA hautafanyika kikamilifu.

5.0 Mapendekezo ya Mbinu za Kukabiliana na Changamoto

Pamoja na changamoto ambazo zimefafanuliwa katika kipengele namba 4, makala haya yanapendekeza mbinu zifuatazo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hizo:

Mosi, serikali na taasisi binafsi zihakikishe upatikanaji rahisi wa vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia kama vile kompyuta, projekta, simu maizi, aipadi na *tabulate* katika maeneo yao yanayohusika na utoaji wa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni. Kuwapo kwa vifaa hivi kutasaidia kupunguza changamoto ya kuwa na vifaa visivyotosheleza idadi ya wanafunzi. Halikadhalika, ili ufundishaji na ujifunzaji ufanyike kwa namna nyepesi ni lazima kuwe na kompyuta zinazoenda na wakati. Hii ina maana kuwa walimu na wanafunzi wanapaswa kuwa na kompyuta ambazo ni za matoleo ya sasa na zenye *window* zinazoendana na wakati husika. Hali hii itasaidia kuepusha ufundishaji na ujifunzaji kukwama. Kwa hivyo, serikali na taasisi binafsi zisaidie kununua vifaa hivyo na kuvisambaza katika vyuo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar na taasisi nyigine kama vile MS TCDC, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Chuo cha Kiswahili na Utamaduni (KIU). Sambamba na hilo upatikanaji wa mtandao wa intaneti na nishati ya umeme wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji ni muhimu kwani utawezesha matumizi ya vifaa hivyo pindi vinapohitajika kutumiwa. Hii ina maana kwamba kwa upande wa nishati ya umeme, serikali isimamie na kuimarisha vyanzo vyote vya nishati ya umeme ili kuwa na uhakika wa kupata nishati hiyo wakati wote, jambo ambalo litasaidia ufundishaji na ujifunzaji kuwa wa uhakika. Ama kwa upande mwingine serikali na taasisi binafsi zinunue majenereta ya ziada ambayo yatasaidia umeme unapokuwa umekatika. Hali hii itasaidia ufundishaji na ujifunzaji uendelee bila kukwama.

Pili, taasisi zinazofundisha Kiswahili kwa wageni kama zilivyoainshwa katika hoja iliyotangulia hapo juu, ziwe na desturi ya kuandaa semina za mara kwa mara zinazohusu namna ya kutumia vifaa vinavyohusika na TEHAMA katika ufundishaji kwa wageni. Hii ni kutokana na kwamba maendeleo ya sayansi na teknolojia yanazalisha vifaa vipya kila wakati, kwa hivyo, ni muhimu pawepo na semina hizo kutoka kwa wataalamu waliobobea katika eneo hilo. Kwa mfano, matumizi ya *power point*, matumizi ya programu za *zoom* na *skype* n.k. Pia, wataalamu hao wafundishe namna ya kutengeneza programu mbalimbali zinazohusisna na ujifunzaji wa lugha kama vile michezo ya lugha inayohusisha vibonzo na chemsha bongo ambayo itasaidia mwanafunzi kuelewa msamiati mbalimbali unaotumika katika mawasiliano ya kila siku. Semina hizi zitasaidia kupunguza changamoto ya matumizi ya vifaa vinavyotumika katika TEHAMA

kwa walimu na wanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni.

6.0 Hitimisho

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya kujifunza lugha ya Kiswahili kuwa makubwa duniani kote, upo umuhimu wa kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha hiyo. Hii ni kwa sababu TEHAMA itasaidia kukisambaza Kiswahili kwa namna rahisi na isiyokuwa na gharama kubwa.

Marejeleo

- Ahmadi, M. R (2018). "The use of Technology in English Language Learning: A Literature Review", *International Journal of Research in English Education (IJREE)*, 3 (2): 115-125
- Bate, A. W. na Poole, G. (2003). *Effective Teaching with Technology in Higher Education: Foundation for Success*. San Francisco, CA: Jossey-Bass
- Bilyalova, A. (2016). ICT in Teaching a Foreign Language in High School, *Procedia-Social and Behavioral Sciences* 237: Kur. 175-181.
- Erben, T. Ban, R. and Castaneda, M. (2009). *Teaching Language Learners through Technology*. New York: Routledge.
- Gençter, B. (2015). How does technology affect language learning process at an early age? *Procedia Social and Behavioral Sciences*, (199), 311316. doi:10.1016/j.sbspro.2015.07.552.
- Korlotyan, D. (2015). "New Technologies in Learning English". Retrieved from <https://prezi.com/d4hdwyeqla5/new-technologies-in-learning-english>.
- Kevogo, S. A. (2017). "Kiswahili katika Kufundishia TEHAMA katika Shule za Msingi Nchini Tanzania: Umuhimu na Changamoto zake", *Kioo cha Lugha* (13) 52-64.
- Korlotyan, D. (2015). "New Technologies in Learning English". Retrieved from <https://prezi.com/d4ehdwyeqla5/new-technologies-in-learning-english>.
- Long, M. (1991). Focus on Form: A Design Feature in Language Teaching Methodology. Katika K. De Bot, R. Ginsberg na C. Kramsch (Wah.), *Foreign Language Research in Cross-Cultural Perspectives* Amsterdam: John Benjamins. Kur. 39-52.
- Lopez, D. (2016). The Use of Authentic Videos, as a Teaching Strategy to Lower Some Boredom Signs shown by Intermediate English Students at the Universidad San Ignacio De Loyola when Practicing Grammar in Order to Improve Results. *Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa)*, Universidad De Piura.
- Mexhuani, A. (2014). *Integrimi I Teknologjisë Informative të Komunikimit në mësimdhënie dhe Nxënie*, Prishtinë, Botim Isntituti Pedagogjik I Kosovës, Teknika.
- Mofareh, A. (2019). The Use of Technology in English Language Teaching, *Frontiers in Education Technology*, 2 (3): 168
- Msigwa A (2019). "Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni". *Mulika*, 38: 74-86.

- Negoescu, A. na Bostina-Bratu, S. (2016). Teaching and Learning Foreign Languages with ICT, *Buletin Scientific*, 21 (1): 21-27.
- Paulsen, J. (2001). "New era trends and technologies in foreign language learning". <http://imej.wfu.edu/articles/2001/1/05/> Accessed 11/05/2013.
- Prensky, M. (2001). Digital Natives, Digital Immigrants, Part 1. *On the Horizon*, 9 (5): 1-6,
- Thorne, S. L. (2010). Intercultural Turn and Language Learning in the Crucible of New Media. Katika F. Helm na S. Guth (Wah.), *Telecollaboration 2.0 for Language and Intercultural Learning* Bern: Peter Lang, Kur. 139-164.
- Tomlinson, B. (2011). *Materials Development in Language Teaching (2nd Ed)*. Cambridge: Cambridge University Press.